# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE.

**MUHUTASARI WA KIKAO CHA DHARULA CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 28/12/2021 KATIKA UKUMBI WA OFISI YA UCHAGUZI.**

**MAHUDHURIO:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Geofrey M. Hamis | Mwenyekiti |
| 2. | Bw. Revocatus W. Shaban | Katibu |
| 3. | Bw. Hashim M. Kazoka | Mjumbe |
| 4. | Bw. Paschal O. Kapinga | Mjumbe |
| 5. | Bw. Yusuph Hamza | Mjumbe |
| 6. | Bw. Aidan M. Frument | Mjumbe |
| 7. | Dr. Theopister Elisa | Mjumbe |

**SECRETARIET**

1. Faraj J. Kampyata

**MUHUT. Na. 01/12/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 3.00 asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao cha siku hiyo.

**MUHT. Na. 02/12/2021 : KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO.**

Wajumbe walisoma na kuthibitisha agenda za kikao cha siku hiyo ambazo zilikuwa kama ifuatavyo;

1. Kufungua kikao,
2. Kusoma na kuthibitisha agenda za kikao.
3. Kuidhinisha njia ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo sita katika Hospitali ya Wilaya ya Sikonge kwa kutumia Force Account.
4. Kuidhinisha njia ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi kama ifuatavyo; Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao makuu ya Halmashauri,ukamilishaji wa maboma shule za msingi na sekondari, ukamilishaji wa Hospitali ya Wilaya na ujenzi wa miundombinu katika shule ya Sekondari ya Nyahua kwa kutumia Force Account .
5. Kufunga kikao

**MUHT. Na. 03/12/2021 : KUIDHINISHA NJIA YA UTEKELEZAJI WA MRADI WA UJENZI WA MAJENGO SITA KATIKA HOSPITALI YA WILAYA NA UKAMILISHAJI WA ZAHANATI KWA KUTUMIA FORCE ACCOUNT.**

Mkuu wa Idara ya Afya aliwasilisha Orodha ya Miradi ya UJenzi itayotekelezwa katika Hospitali ya Wilaya na Zahanati. Wajumbe kwa pamoja walijadiliana na kukubaliana kwamba

CamScanner

miradi hii itekelezwe kwa kutumia njia ya Force Account kama maelekezo/ Mwongozo wa miradi hiyo unavyotaka.
Orodha ya miradi ni kama ifuatavyo;

1) Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Tsh. 800,000,000.00
2) Ujenzi wa Jengo la Dharula(EMD) na Nyumba ya Watumishi Tsh. 390,000,000.00
   Baada ya wajumbe wa Bodi ya Zabuni kwa pamoja kupitia ripoti ya tathmini na kupitia maelekezo yaliyotolewa na serikali juu ya miradi hii, kwapamoja walikubaliana kuwa miradi hiyo itekelezwe kwa njia ya Force Account kwakuwa mkandarasi ameomba kufanya kazi hiyo kwa gharama ya juu sana inayozidi pesa iliyotolewa na serikali. Pia kwa upande wa nyumba ya watumishi wajumbe pia waliridhia njia ya Force Account itumike kwakuwa mkandarasi aliyenunua kitabu cha zabuni hiyo hakurudisha kitabun hicho.

3) Ukamilishaji wa Zahanati ya Mwamayunga Tsh. 50,000,000.00
4) Ukamilishaji wa Zahanati ya Kidete Tsh. 50,000,000.00

**MUHT. Na. 04/12/2021: KUIDHINISHA NJIA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBALIMBALI YA UJENZI KAMA IFUATAVYO; UJENZI WA JENGO LA OFISI YA MAKAO MAKUU YA HALMASHAURI, UKAMILISHAJI WA MABOMA NA MAABARA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI NA UJENZI WA MIUNDOMBINU KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA NYAHUA KWA KUTUMIA FORCE ACCOUNT.**

Mkuu wa Idara ya Mipango na Uchumi aliwasilisha Orodha ya Miradi ya UJenzi itakayotekelezwa katika ngazi ya Shule za Sekondari, Shule za Msingi na Jengo la Ofisi makao makuu. Wajumbe kwa pamoja walijadili na kuidhinisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa njia ya 'FORCE ACCOUNT'.
Orodha ya miradi ni kama ifuatavyo;

A. UKAMILISHAJI WA MABOMA SHULE ZA MSINGI
   1) Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Chang'ombe Tsh. 25,000,000.00
   2) Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Ipembe Tsh. 25,000,000.00
   3) Ukamilishaji wa Chumba kimoja cha Darasa Shule ya Msingi Mole Kiloleni Tsh. 12,500,000.00
   4) Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Mwitikio Tsh. 25,000,000.00
   5) Ukamilishaji wa vyumba viwili vya madarasa Shule ya Msingi Tulieni Tsh. 25,000,000.00

B. UKAMILISHAJI WA VYUMBA VYA MAABARA SHULE ZA SEKONDARI
   1) Ukamilishaji wa chumba cha Maabara Tutuo Sekondari Tsh. 30,000,000.00
   2) Ukamilishaji wa chumba cha Maabara Ngulu Sekondari Tsh. 30,000,000.00
   3) Ukamilishaji wa chumba cha Maabara Igigwa Sekondari Tsh. 30,000,000.00
   4) Ukamilishaji wa chumba cha Maabara Usunga Sekondari Tsh. 30,000,000.00
   5) Ukamilishaji wa chumba cha Maabara Msuva Sekondari Tsh. 30,000,000.00

CS CamScanner

C. UKAMILISHAJI WA MABOMA SHULE ZA SEKONDARI

1) Ukamilishaji wa boma la chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari ya Chabutwa Tsh. 12,500,000.00
2) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba viwili vya madarasa Shule ya Sekondari ya Kamagi Tsh. 25,500,000.00
3) Ukamilishaji wa boma la chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari ya Kiloli Tsh. 12,500,000.00
4) Ukamilishaji wa maboma ya vyumba viwili vya madarasa Shule ya Sekondari ya Kipili Tsh. 25,500,000.00
5) Ukamilishaji wa boma la chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari ya Kisanga Tsh. 12,500,000.00
6) Ukamilishaji wa boma la chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari ya Langwa Tsh. 12,500,000.00
7) Ukamilishaji wa boma la chumba kimoja cha darasa Shule ya Sekondari ya Usunga Tsh. 12,500,000.00

D. UJENZI WA MIUNDOMBINU YA SHULE YA SEKONDARI NYAHUA

Ujenzi wa miundo Mbinu shule ya Sekondari Nyahua Tsh. 470,000,000.00

E. UKAMILISHAJI WA JENGO LA OFISI MAKAO MAKUU

Ukamilishaji wa gholofa ya kwanza katika jengo la Ofisi Makao Makuu Tsh. 750,000,000.00

**MUHUT. Na. 05/12/2021. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alitamka kufunga kikao mnamo saa 4:00 Asubuhi

**UMETHIBITISHWA:**

Cheo: **Mwenyekiti**
Saini..................
Tarehe 28/12/2021

Cheo: **Katibu**
Saini: ..................
Tarehe 28/12/2021

CamScanner